SHULE YA SEKONDARI NZIVI,
S.L.P. 29,
MUFINDI.

11/12/2020

SIMU 0769162020/0786408746 (MKUU WA SHULE)

0756070236(MAKAMU MKUU WA SHULE)

KUMB: NA. NZIVI SS/JI/VOL.I/13

Kwa,
Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi:-

.....

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NZIVI MWAKA 2021

Uongozi wa shule ya sekondari Nzivi unayo furaha kukuarifu kuwa mtoto wako ..... mwenye namba ya mtihani ..... amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Mtoto wako anatakiwa afike shuleni saa 1:30 Asubuhi siku ya Jumatatu ya tarehe 11/01/2021 tayari kwa kuanza masomo.

Hii ni shule ya kutwa, mtoto atarudi kuishi nyumbani kwako siku zote au unaweza kupanga nyumba zilizo karibu na shule. Aidha mtoto wako atapokelewa kwa malengo ya kuwa ataendelea na masomo hadi kidato cha nne. Haitakiwi mtoto wako kukatishwa masomo, vinginevyo sheria itachukua mkondo wake kwa yeyote atakaye husika kufanya hivyo.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ipo katika kijiji cha Nzivi, kitongoji cha Mtwango, upande wa kulia ukitokea Igowole kuelekea Nyololo au upande wa kushoto ukitokea Nyololo kuelekea Igowole.

A: MAMBO YA MUHIMU YA UTEKELEZAJI KWA MWANAFUNZI

1. Mkoba mweusi wa kubebea madaftari
2. Daftari kubwa zisizopungua 10 (QUIRE 3)
3. Mkebe 1(mathematical set)
4. Faili kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi(1)
5. Fagio aina ya chelewa kwa ajili ya kufanyia usafi 2
6. Ndoo moja ya lita kumi kwa ajili ya kufanyia usafi na shughuli nyingine kama vile kumwagilia bustani

B: SARE YA SHULE:-

i) WASICHANA:-

1. Sketi ndefu (ivuke magotini) ya heshima ya rangi ya bluu nyeusi(2)(**dark blue**) mshono wa rinda boksi mbele na nyuma
2. Mashati meupe mikono mirefu (2)
3. Tai ya rangi ya bluu nyeusi (dark blue) ni **LAZIMA**
4. Soksi nyeupe (pea 2)
5. Sweta rangi ya bluu nyeusi (dark blue) ni lazima iwe na muundo wa **v** shingoni
6. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba (visivyo na kisigino kirefu)
7. Traksuti kwa ajili ya michezo rangi ya bluu bahari
8. Raba kwa ajili ya michezo

ii) WAVULANA

1. Suruali ya heshima rangi ya bluu nyeusi (dark blue) isiwe ya mtumba(2)
2. Mkanda wa suruali mweusi
3. Soksi rangi nyeusi (pea 2)
4. Mashati meupe ya mikono mirefu (2)
5. Tai ya rangi ya bluu nyeusi (dark blue) ni **LAZIMA**
6. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba
7. Sweta rangi ya bluu nyeusi (dark blue)ni **LAZIMA iwe na muundo wa V shingoni**
8. Traksuti kwa ajili ya michezo rangi ya bluu bahari
9. Raba kwa ajili ya michezo

C: VIFAA VINGINE:-

1. Picha ya passport nakala 1
2. Dictionary ya kiingereza
3. Kamusi ya Kiswahili

NB: VIFAA VYOTE VITAKAGULIWA

D: FOMU ZA KURUDISHA SHULENI:

- ✓ Taarifa binafsi za mwanafunzi
- ✓ Hati ya daktari
- ✓ Kukubali kufuata sheria za shule

UNAKARIBISHWA KATIKA SHULE HII

.....

REHEMA MGONGOLWA
MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI NZIVI

SHERIA ZA SHULE

1. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule wakati shughuli isipo kuwa kwa kibali cha mwalimu wa zamu au mwalimu mwingine
2. Sare ya shule itavaliwa wakati wote wa shughuli za shule
3. Atatakiwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama ilivyopangwa katika ratiba
4. Atasimama mara moja na kumsalimia ipasavyo mwalimu,mfanyakazi wa shule au mgeni aliyemzidi umri anapopita ,anapoingia darasani au kwenye mkusanyiko wa wanafunzi
5. Ataitika mara moja na kukimbia aliko kiongozi aliyemuita
6. Atatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote wa shule ambao ni walezi wake
7. Haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kwa wanafunzi wenzake, walimu, au mtu yeyote Yule
8. Atatakiwa kushirikiana na kusaidiana na wenzake katika kazi
9. Sehemu zifuatazo ndani ya shule zinakatazwa kuingia isipokuwa kwa kibali maalumu:- ofisi za shule,maabara,nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu na jikoni
10. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo wakati wote wa uanafunzi wake: vilabu vya pombe, majumba ya starehena majumba ya kufikia wageni (guest house)
11. Kwa muda wote wa uanafunzi wake haruhusiwi kufanya yafuatayo
    a) Kuvuta sigara
    b) Kunywa pombe au kutumia kileo cha aina yoyote ile
    c) Kufuga ndevu
    d) Kusuka nywele (kwa wasichana)
    e) Kufuga kucha
    f) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima au kuvaa kofia katika eneo la shule
    g) Kugombana na kupigana
    h) Kunyoa nywele kihuni (nywele zilingane)
    i) Kumiliki na kutumia simu ndani na nje ya eneo la shule
12. **Makosa yafuatayo yanaweza kumsababishia mwanafunzi kufukuzwa shule**
    - **Wizi**
    - Uasherati
    - Ulevi wa aina yoyote
    - Uvutaji bangi
    - Kupigana
    - Makosa ya jinai
    - Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
    - Kuchana bendera ya serikali au picha za viongozi wa serikali, kudharau bendera au wimbo wa Taifa
    - Kushiriki katika magendo, kamari au ujangili
    - Kupata, kumpa na kutoa mimba
    - Kuanzisha, kuongoza, kuchochea,kushiriki ghasia,vurugu au mgomo wowote wa wanafunzi

MWISHO: Tunamtakia mwanao afya njema na mafanikio wakati wote uanafunzi wake

.....

REHEMA MGONGOLWA

MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI NZIVI,
S.L.P. 29,
MUFINDI.
11/12/2020

1. Mimi ..... niliye chaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha ..... katika shule ya sekondari Nzivi ninaikubali nafasi hiyo. Ninaahidi kuwa nitafuata sheria zote za shule zilizopo na zitakazo kuja baadaye. Nitajiepusha na vitendo vyote ambavyo ni kinyume cha sheria na taratibu za shule. Nitakuwa mtiifu kwa walezi wangu wote shuleni ambao ni walimu na wafanyakazi wasio walimu
2. Nitafuata maelekezo nitakayopewa na walimu na wafanyakazi wengine wa shule na viongozi wote watakaokuwepo kwa mujibu wa sheria
3. Naahidi pia kuwa nitatumia uwezo na akili yangu kwa juhudi kubwa ili kupata mafanikio na matokeo mazuri katika masomo yangu
4. Nitahudhuria vipindi vyote vya masomo na nje na nitafanya mazoezi ya mitihani yote nitakaayopewa
5. Ninafahamu kwamba kukiuka ahadi hii kutanipotezea ahadi ya masomo

Sahihi ya mwanafunzi ..... Tarehe .....

Jina la Mzazi/Mlezi ..... Tarehe .....

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ..... Tarehe .....

IMESIMAMIWA NA

.....

REHEMA MGONGOLWA

MKUU WA SHULE

PRESIDENT'S OFFICE-RALG

MUFINDI DISTRICT COUNCIL

MEDICAL EXAMINATION FORM

NZIVI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 29
MUFINDI
11.12.2020

THE MEDICAL OFFICER

.....

.....

RE:MEDICAL EXAMINATION IN RESPECT OF .....

I would be very grateful if you would kindly examine the above named student as to her/his fitness for admission to school as a day secondary Education under the list below:

Head of school

Examine and certify the following items

1.EARS .....

2.EYES .....

3.BLOOD COUNT .....

4.SPLEEN.....

5.CHEST .....

6.STOOL .....

7.URINE .....

8.T.B .....

9.TYPHOD .....

10. S.T.D .....

11.PREGNANCE .....

12.Any physical/mental defects or impairment identified .....

.....

13.Any additional comments:.....

.....

I have examined the above named and consider him/her fit/unfit for admission to pursue secondary studies.

....

DATE MEDICAL OFFICER'S SIGN & STAMP